simulizi fupi

# Kikao cha haki



Godlove Kabati

# KIKAO CHA HAKI

*Simulizi fupi*

**Godlove Kabati**

**2024**

# UTANGULIZI

*“Haujawahi kuwa mchezo salama kabisa.*

*Ni mchezo ambao kama ukiucheza na haujui kanuni zake…basi utapata majuto  na maumivu.*

*Wengi wameutungia nyimbo na mashairi, tukayaimba.*

*Wengine wameuandikia hadithi na riwaya, kwa lugha nzuri za kifasihi na sarufi, tukazisoma.*

*Hawa wengine wameuigizia tamthilia na filamu, tukazitazama.*

*Lakini bado hatukupata maana halisi na jibu la huu mchezo.*

*Ni kama fumbo gumu ambalo halijawahi kuwa rahisi kufumbua. Ni kitendawili kigumu ambacho hata ukipewa mji uende na urudi na majibu yake bado ungeshindwa tu.*

*Ni mchezo wa mapenzi.*

*Yaliyowakuta hawa wapendanao wawili, kila mmoja akiwa na hoja zake- hadithi za kusikilizwa. Kilifanyika kikao…*

*Hatutamlaumu mwanamke baada ya kuisikiliza hadithi ya upande mmoja tu wa mwanaume. Tutataka kuisikiliza pia hadithi ya mwanamke.*

*Hii ndio haki”*

G.Kabati

# 1

( MWAMUZI)

Naam mista Ansbert,

Umeniita hapa ili niwe mwamuzi wa mgogoro wenu: wewe na huyu aliyekuwa mpenzi wako…Nadia.

Nadhani ni wasaa mzuri kabisa wa kuisikiliza hadithi yako na baadae tutasikiliza upande wake.

Haya karibu utusimulie ni namna gani mlikwaruzana na ilikuwa vipi.

******

(MWANAUME)

Asante sana, kwa kuwa umeshanitambulisha kwa jina, sidhani kama itakuwa sahihi kwangu kutumia sekunde kadhaa kuwaaminisha watu juu ya jina hili.

Eeer,

Hapo mwanzo mimi na Nadia tulipendana sana. Sikuwahi kufahamu ni shida gani kubwa iliyotokea…lakini mimi na yeye tuliwahi kupendana sana.

Tulikuwa vizuri tu hapo mwanzo. Narudia tena kwa mara nyingine, tulipendana sana tena sanaaa.

Mapenzi yetu yalifaa kabisa kuwa kama kivutio cha utalii, watu wengine waje washuhudie kwetu maana halisi ya kupendana.

Tulienda vacation mbalimbali…tulivaa sare, tukazuru maeneo na vivutio mbalimbali hapa nchini na nchi kadhaa za nje.

Nikampatia na ahadi nyingi…

"Baby, mwakani tutaenda Philadelphia. Au haupapendi twende tukale raha mji wa Miami?"

Akajibu kuwa hapendi kwenda Amerika, anataka kwenda Dubai. Tayari rafiki zake wameshamsimulia juu ya maajabu ya uzuri wa mji huo mkubwa wa kibiashara.

Mi' nikamkubalia, nilitaka daima mimi nisiwe chanzo cha huzuni yake. Bali niwe chemchemi ya furaha yake. Unadhani nilifanya hayo tu?

Hata alipohitaji attention yangu nilimpatia. Muda wowote ule simu yangu ilipounguruma na nikaona lile jina nililomsevu la kimahaba, *'corazon'* niliwahi fasta kuiokota…haijalishi ulikuwa ni ujumbe au alinipigia.

Kama simu yangu ingepata nafasi ya kuwa hai, nadhani ingeweza kuwa shuhuda wa wingi wa sekunde zote na dakika nilizowahi kuwasiliana naye.

Ingewaeleza juu ya zile meseji nzuri na tamu zilizoundwa kwa herufi na silabi za mapenzi…zilizopambwa kwa emoji na maua. Ingewashuhudia juu ya zile saa tulizokaribishana mbele ya kila sahani yenye chakula, ingewaelezea juu ya kuulizana kwetu kama kila mmoja ameshakula.

Hii simu hii,

Ingelalamika juu ya ule muda mrefu wa maongezi ambao niliutumia usiku kuongea naye, sauti yake ikiwa nyororo na ya kubembeleza na ya kwangu ikiwa nzito na iliyotangaza usalama. Mwisho wa maongezi kila mtu angesusa kukata simu. Kila kitu kimebadilika, leo hii kila mtu amesusa kuliona jina la mwenzie kwenye orodha ya contacts.

Kuna imani kuu kwetu wanaume, inayosema kuwa ni nguvu ya pesa yenye uwezo wa kumuonesha mwanamke ni namna gani unampenda.

Hata mimi nilikuwa mmoja kati ya waamini wa imani hii. Kwangu pesa niliiiona kama mbolea inayostawisha penzi katika shamba la mahusiano yangu mimi na yeye Nadia. Basi niliiongezea fedha kwenye hili shamba langu.

Ni kweli mimi sio tajiri sana. Lakini kwa kila nilichokipata nilijitahidi sana kumtimizia mahitaji yake

yote. Nilijitahidi sana kufanya kazi na kuongeza kipato change ili tu kukidhi haja zake yeye.

Sijui atanilaumu kwa lipi.

Kitandani? Nilikuwa rijali kwelikweli. Nilimridhisha! Tena akawa ananisifia sana.

Lakini alibadilika ghafla sana, akawa mwenye hasira kila muda, akaanza kutegea kunitafuta.

Kuna siku nilimpigia simu akawa anaongea harakaharaka kuwa yuko bize. Na mimi nikajipa imani kuwa labda alikuwa bize sana na kazi mchana, nitamtafuta usiku. Lakini huu ubize wake mchana ulikuwa wa ghafla sana.

Nilipigwa na mshtuko kuwa kumbe hata nilimpompigia usiku akanambia kuwa amechoka sana. Na wala hakuniambia 'nitafute kesho', alinambia kuwa 'tutawasiliana siku nyingine…'

Ajabu iliyoje!!

Nadia ndio wa kuniambia mimi hivyo! Lakini kumbe sikujua kuwa mimi ndiye nilikuwa nyuma ya muda. Kuanzia hapo nikawa nimemkaribisha shetani kwenye penzi letu. Tena nikamkaribisha chumbani kabisa nikamtandikia na kitanda.

Huyu shetani akawa amelichafua penzi letu mimi na Nadia. Nadia alibadilika sanaa, akakauka kabisa! Zile meseji za mahaba zikageuka meseji za kashfa na

malalamiko. Ikawa sasa kila mtu anajali tumbo lake bila kuwaza mwingine amekula nini.

Kila kitu kilipotea upesi sana kama barafu iliyoanikwa kwenye jua la jangwani. Upendo wetu ukaanza sasa kuwa uadui. Ilikuwa ni kama tunatafutiana kosa ambalo lingetufanya tuachane.

Nikahisi labuda nimekosea sehemu…lakini sikuona kosa langu. Labda kwa vile alijua kuwa nampenda sana nd’o sababu akanifanyia visa vyote hivi.

Kama maajabu tu, mimi na Nadia tuliachana bila hata kupeana taarifa. Alipotea mbele yangu na mimi nikapotea kwenye maisha yake. Mawasiliano yakakatika.

Nafsi yangu ikamezwa na hisia za hasira, nilimchukulia Nadia kama amezidharau sana juhudi zangu. Nikaamua kumlipizia kisasi. Kisasi ambacho ilibidi aone kwa macho yake na atambue kwa ubongo wake.

Kauli niliyoiita ya kishujaa ikanitoka kinywani mwangu,

“There is plenty of fish in sea”. Kuwa samaki ni wengi sana kwenye hii bahari…na mimi kama mvuvi nisiwe na hofu maana bahari ni kubwa mno. Sikutaka ushauri, nikavua samaki wengine kutoka baharini.

Nilianza kujihusisha kwenye mahusiano na mabinti wengine tena wengi. Na kwa kasi sana nikataka kumvimbia kwa makusudi Nadia mpaka ajue.

Atajuaje sasa?

WhatsApp status…kule ndiko kulikuwa bandari ambayo nilitia nanga ya hisia zangu zote na maumivu juu yake.

Nikacheza na settings…aone yeye peke yake. Namna nilivyoteketeza pesa kununua vinywaji vya bei ghali…mimi na warembo wengine tukala bata kiasi cha kuku kuona wivu. Nikiandika caption za vijembe na mafumbo kumsuta yeye tu. Kiukweli nilimtumia mishale mingi ya sumu hukohuko mitandaoni.

Lakini yote haya nilifanya  nikiwa na giza moyoni mwangu. Bado Nadia alikuwa na nafasi kubwa kwenye moyo wangu. Alikuwa ameweka makazi ya kudumu kwenye moyo wangu.

Nilikuwa naishi kwenye ndoto ya kuwa akiniona, ataona wivu…labda atanirudia. Ataniomba msamaha na kuacha hizi tabia zake zote za maudhi. Nilikuwa najipa matumaini bila hata ya kujua huko aliko anatembea na nani, yuko na nani kwenye mahusiano yake mapya.

Nilichokijua mimi ni kuwa upendo wake kwangu umepungua kwa kuwa amempata mtu mwingine. Bosi labda au kibopa mwenye pesa katika kazi zake za uhasibu.

Mimi nikaendelea kujijengea tulizo la nafsi ambalo lisingeniponya jeraha la moyo wangu. Pombe inapunguza mawazo na maumivu kwa muda tu…lakini iishapo kichani matatatizo yanabaki palepale.

Sikupata faraja yoyote ile, bado ilikuwa ngumu kumtoa akilini mwangu…alikuwa kama sumu iliyotapakaa kwenye mfumo wa damu yangu.

# 2

(Ushahidi wa mwanaume)

Mimi ni mjasiriamali. Ninamiliki migahawa kadhaa hapa jijini.

Siku moja nikiwa kazini, nilipokea simu  kutoka kwa rafiki yangu akaniambia kuwa niwahi haraka sana katika hoteli fulani kubwa hapahapa jijini Dar-es-Salaam. Akaniambia kuwa kuna kioja cha kutazama na sio kusimuliwa.

Nikaziahirisha shughuli zangu zote nikawasha gari yangu na kuwahi eneo nililoambiwa. Nilipofika nje, rafiki yangu akanielekeza ndani katika meza aliyokuwa amekaa na nilipotulia tu hakutoa salamu wala kuhiataji kujua hali yangu... akanambia nigeuke nyuma na niangalie upande wa kushoto. Nikageuka!

Macho yangu ya nyama yaliona vizuri sana. Haukuhitajika msaada wa miwani ya lenzi au hadubini ya kisayansi…niliyemuona pale alikuwa ni Nadia, hakuwa peke yake- alikuwa na yule mwanaume aliyewahi kuniambia kuwa ni rafiki yake tu.

Na yeye so kwmaba hakuniona…aliniona pia. Lakini kwa macho ya dharau na kiburi tena kiburi cha kiwango cha lami…akanicheka!

Maajabu!

Macho yangu yalikuwa yanashuhudia kioja cha taswira. Nadia alikuwa na jamaa yake. Huyu jamaa sura yake haikuwa ngeni. Picha yake iliwahi kutundikwa na Nadia kwenye status akidai kuwa ni rafiki yake. Na mimi sikutaka kumghasi sana kipindi kile, nilikubali kishingo upande, sumu ya wivu ikiuteketeza moyo wangu.

Mwamba huyu hapa!

Jamaa alikuwa amekamilika kwelikweli; bila kutafuta ushahidi mwingi sana…hela ilionekana ipo pale!

Mwili wake wa mazoezi ulitangaza ushupavu, ulivikwa mavazi nadhifu ya gharama, kwa kumkagua nilimkadiria kuwa kavaa laki tano hivi kama sio sita. Saa yake mkononi tu ilipigilia msumari utajiri wake, NAVY FORCE brand ya kwanza kabisa.

“Oa bro! si Nadia yule au?” Rafiki yangu alinitupia swali ambalo hata yeye jibu alikuwa nalo, tashtiti hii ilinishtua katika mawazo yangu nikiwa bado nimegeuka nyuma macho yangu yametupwa katika ile meza alipokuwa Nadia.

Sikujua nimjibu nini. Ulimi wangu mzito, mdomo wangu mchachu- mate yamenikauka kama nimepigwa

ganzi. Hasira iliyochanganyikana na wivu, vilichemka sana mwilini mwangu.

Mikono yangu ilinitetemeka sana kwa hasira kiasi kwamba hata jasho jembamba lilinitoka kwenye viganja vya mikono yangu.

Hata muhudumu aliyekuja kunihudumia, sikumsikia kwa wakati huu. Masikio yangu yalikuwa yametiwa uziwi.

“Kaka uletewe nini?!” alinishtua rafiki yangu.

“Si-si-sidhani kama nitatumia chochote kwa sasa…asante!” ilinitoka.

Muhudumu akaanza kuzihesabu hatua zake kutoka pale mezani. Halafu ukavu wa koo langu ukanikumbusha kuwa nahitaji maji.

“Mu-muhudumu!! Dada!! Tafadhali niletee maji ya kunywa!”, ikanibidi nimuite kwa sauti tena yule muhudumu. Sikueleweka! Kama nilihitaji huduma au sikuhitaji.

Niliwatazama Nadia na mpenzi wake, nikiwa nakunywa maji kupunguza hasira na kiu. Sikuwa na cha kufanya. Nilikuwa kama mbwa mkali aliyefungiwa kwenye banda imara, anawaona wezi na kuishi kubweka tu.

Nadia akazidisha mapozi..akawa anamtazama yule bwana kwa kulegeza macho. Anajichekesha , mbaya zaidi akainamisha kichwa chake na kumpiga busu zito.

Dharau nyingine hii!!

Tena mbele yangu. 'Anafanya makusudi huyu ili uumie!'.

"Oyah Bruno!" Nilimuita rafiki yangu ambaye muda wote huu alikuwa ametulia tuli akiburudika na sod yake ya Pepsi baridi.

"Nipange mwanangu"

"Huu ni u$#%* naenda kuwawashia moto!!"

Tusi kali lilifyatuka nikimtangazia rafiki yangu juu ya balaa ambalo ningeenda kulizua pale mezani kwa Nadia.

"Tulia babuh! Sasa demu si mliachana kitambo? We shida yako nini sasa. Ulitaka kujua anatoka na nani…nimekuita hapa ujionee homie"

"Aah hii haivumiliki mwanangu" . Hisia za hasira ziliendelea kunitawala.

"Poa kama vipi tuondokee sasa. Tayari nimeona upuuzi niliotaka kuona. Nikiendelea kukaa hapa nitampasuapasua huyu manzi kudadek!"

“Em tuliza hilo povu…tusepe sasa” alimalizia soda yake kwa mafundofundo na tukaondoka pale.

Sikutaka kugeuka nyuma tena. Tayari dharau alizonionyesha Nadia zilinitosha, sikutaka zaidi.‘Ina maana muda wote ule walikuwa kwenye mahusiano?’. Bado akili yangu iligoma kuamini.

Niliingia kwenye gari mimi na rafiki yangu, nikamuachia usukani aendeshe yeye maana nisingeweza kuendesha kwa wakati ule.

Aliendesha akinishauri na kunisemesha maneno mengi ya faraja na hekima ambayo sikuyasikiliza kwa makini, niliyaona yote kuwa ya kipuuzi tu. Yasingeweza kubadilisha ukweli wowote ule kuwa Nadia aliniacha na kuchukuliwa na yule aliyewahi kuniambia kuwa ‘ni rafiki tu’.

Jambo la maana zaidi lililofanywa na maneno yake ni kupasua lile anga la ukimya ndani ya gari. Maneno pekee niliyoyasikia,

*“...hawa wanawake ni nyoka kaka!..”*

Siku ilikuwa imeanza vizuri kazini, ghafla ikawa siku mbaya kazini. Niliwahi kurudi mapema nyumbani kwangu.

Kila ujumbe ulioingia kwenye simu yangu niliuona ni kama ukinicheka kiwango cha ubwege nilio nao. Sikujishughulisha kuujibu, hata kama ungehusisha neno *'pesa'*.

Kila kinywaji kitamu nilichokizoea kilikuwa kichungu mdomoni mwangu. Hakukuwa na pombe yoyote ambayo iiwhai kuondoa jina Nadia akilini mwangu, hivyo niliacha kunywa pombe tangu zamani.

Nikamkumbuka yule jamaa aliyekuwa na Nadia kule hotelini, nikajilinganisha naye,

"Amenizidi nini kwani yule. Labda kanizidi kujali sana eeh?! Lakini huyu Nadia huyu.." nikajiuliza mimi mwenyewe. Mishale ya saa pale ukutani ilielekeza kuwa wakati huo ulikuwa ni saa moja na nusu jioni.

Nikaokota simu yangu iliokuwa juu ya meza, nikaanza kuitafuta namba ya Nadia ambayo nilikuwa nimeiblock. Mara chache sana nilikuwa naitumia hasa nikitaka kupost status za vijembe au kutegeshea kama nitapata ujumbe wowote ule kutoka kwake. Nilikuwa nimeifuta mara kwa mara na kuisevu tena. Maana nilikuwa nimeikariri tayari.

Nikaipiga! Ikaita …'alaa kumbe hakuniblock?', nikashtuka

Nikapata lepe la wasiwasi, ‘Huyu anaweza akahisi kuwa bado nampenda labda’. Moyo ukasita nikataka kukata simu, lakini nikakaza!

Simu ikaita weee…hadi ikakata! Nikavuta pumzi ndefu. Niliogopa sana kuwa atanifikiriaje huyu binti?

Nikavaa ujasiri, nikapiga tena ile namba…haikuita sana, ikapokelewa!

“Haloo?!”, ilikuwa ni sauti nyepesi ya kike, sauti ambayo nilikuwa nimeizoea japo sikuwa nimeisikia kwa muda mrefu sana. Sauti ya Nadia!

“Haloo Nadia! Habari yako?!”, nilimjibu kwa sauti baridi, sauti iliotangaza simanzi.

“Poa mzima wewe?!...”

“Safi aisee za masiku?”….nikazidi kumjulia hali, bado sielewi nianze na mada gani.

“Poa tu…naongea na nani mwenzangu?”

Japokuwa ilikuwa sauti nyororo lakini hili swali lilinichoma kama kisu kikali tumboni mwangu. Nadia hakuwa na namba yangu! Amenisahau.

Sekunde kadhaa zikapita nikiwa kimya.

“Haloo?” akaniita.

“Mimi..mi. ni Ans, Ansbert hapa!”, nilimjibu kwa kigugumizi.

“Eeh wewe…vipi?” sikujua kama aliniuliza swali ama alikuwa akinishangaa.

“Eeer, uko poa?” nikazidi kumuuliza maswali kutaka kuifahamu hali yake, nilijipanga kutaka kutoa sumu zangu.

“Nakusikiliza…” alinijibu kwa dharau.

“Nadia yule uliyekuwa naye leo ni nani?”, lilikuwa swali langu la moja kwa moja kwake. Jibu nilikuwa nalo moyoni na sikupenda kuamini moja kwa moja mpaka pale ambapo yeye mwenyewe anijibu.

“Kwani we  umeonaje? Na unaniuliza kama nani?”

Dharau!

Kauli yake ilinichoma kama mkuki wa moto.

‘Huyu demu kapata wapi hizi kauli za kibabe?’, niliwaza. Na katika shangaa yangu hiyo akanitupia jibu la moja kwa moja,

“Kwa taarifa yako…uliyemuona ni mume wangu mtarajiwa! Mwezi ujao unakaribishwa harusini, upo hapo!”

Ajabu nyingine!

Kauli yake ilibeba kila aina ya maneno ya hasira, chuki na makasiriko. Sikumbuki mara ya mwisho Nadia kuongea kwa hasira namna hiyo ilikuwa lini.

Lakini leo hii amenipatia mwaliko usiokuwa na kadi. Kuwa nakaribishwa kwenye harusi mwezi ujao. Mimi nilidhani kuwa yule bwana alikuwa mpenzi tu, kumbe alikuwa ni mchumba kabisa. Nilikuwa nimepotea njia!

Huu ulikuwa ni ukweli mchungu sana kuumeza. Mwili wangu ulizizima.

'Nimjibu nini huyu?' nilijiuliza. Ni kweli kuwa nilichukizwa na maneno haya ya Nadia, lakini nilichelea sana yeye ajue kuwa amenikasirisha.

"Ooh! Hongera sana. Hivi nd'o umesema kuwa harusi ni mwezi ujao eeh? Safi sana. Nitafurahi sana kama nitapata kadi ya mwaliko." nilitamka nikiwa nimejikaza kisabuni tena kwa sauti tulivu mno iliyoonyehsa kuwa sikustaajabishwa na harusi ile. Nikamsikiliza kuwa atajibu nini,

Akakaa kimya kidogo kisha akanijibu,

"Aasanteh…nitakutumia tu wala usijali. Vipi lakini mawifi wangu hawajambo?", ilimtoka.

Mtego huu! Nilishtuka tena

Sasa Nadia alitaka kutumia bomu lilelile nililotumia mimi. Alitaka wote tuonekane tuna makosa. Lakini mimi sikutaka kunasa humo,

“Uum…nakumbuka uliwahi kuniambia kuwa ni rafiki yako huyo bwana…vipi lakini anaitwa nani?”

Kabla hajanijibu, nikasikia purukushani kwenye simu. Ni kama Nadia alikuwa bize na mtu fulani huko alikokuwa.

Nikasikia kwa mbali ni kama sauti nzito ya kiume imeingia eneo lile, na kweli hali ya hewa huko ikawa ni kama imechanganywa kwa sauti mbili ya kike na ya kiume. Mimi nilitambua hii ya kike kuwa ya Nadia, lakini ya kiume la sikuitambua mara moja.

Nikasikiliza sauti za vicheko na mabusu kadhaa. Ndio hakukata simu yangu lakini hii dharau ya kuniacha hewani na kujishughulisha na mwanaume mwingine kilikuwa ni kiwango kikubwa mno cha dharau kwangu.

‘Nani huyu kama sio yule bwana mume mtarajiwa?’ Nilijihoji.

“Darling ongea na huyu hapa…msalimie” nikasikia sauti ya Nadia ikibembeleza ombi kwa huyu jamaa aliyeitwa ‘Darling’.

“Hey haloo!” sauti nzito ya kiume ilisikika ikiutambua uwepo wangu katika simu ile iliyokuwa imesuswa na Nadia.

Ilikuwa sauti ya mamlaka haswahaswa, sawa na mfalme aliyekuwa katika milki yake. Niliganda kama sanamu, mishale na mikuki ya sumu ambayo Nadia alinitupia haikumtosha, sasa alikuwa akitumia silaha za nyuklia kuniangamiza kabisa!

“Haloo bro! niaje?” nikamjibu.

“Kama kawa mzee niaje hapo?” jamaa akanijibu,

“Kwema sana kaka, mishe vipi?”

“Sana tu…nani hapo?!”

‘nani hapo’? ningejitambulisha kama nani? Rafiki yake Nadia? Hapana ningekuwa nimejishusha sana. Kaka basi?! Nilitaka kujizaba kofi baada ya kufikiria hivi tena. Kaka? Yaani mimi niwe kaka yake Nadia.

Hapana. Nilipata kigugumizi cha ghafla. Mimi ni nani kwa Nadia? Sio mpenzi, sio ndugu, sio rafiki nikisema mimi ni ex tena kwenye masikio ya mwanaume mwenzngu nitakuwa kichekesho.

Lakini yote haya ya nini…nimepiga simu kwa Nadia ili nijue nini ambacho sikijui? Kila ukweli mchungu

niliotak kudhibitisha nilikuwa nao mezani tayari. Nilijiona punguani sana.

“Haloo ka-…” kabla hata hajamalizia sentensi yake nikakata simu na kuitupa  juu ya sofa.

“Mimi ni fala sana!”nilijikuta nikijisemesha mwenyewe, nikayasindikiza maneno yangu kwa glasi ya kinywaji nilichokiona ni kichungu hapo awali. Wakati huu kilikuwa kitamu sana.

“Bonge la falaa!!” Nikatamka tena kwa sauti baada ya kumeza fundo lile la kinywaji. Nadia alikuwa amenifanya zuzu. Upendo mwingi niliokuwa nao juu yake ulikuwa kama gereza la maisha yangu. Gereza lililonifanya nisikubaliane na uhalisia kuwa yeye sio wangu tena. Ameenda!

Tayari alikuwa ameshinda huu mchezo, tena kwa magoli matatu bila. Na mimi sikutaka nimuonyeshe kuwa nashindana naye, sikutaka afahamu kuwa naumia kwa kushinda kwangu.

Kila kitu hupungua thamani pale kinapokuwa na machaguo yake ya ziada. Mimi kwa Nadia nilikuwa chaguo la mwisho kabisa. Alikuwa amepata kilicho bora kwake.

Hiyo ndio ilikuwa siku yangu ya mwisho kuisikiliza sauti ya Nadia na ikawa siku ya kwanza kumuepuka na kujifunza kumsahau.

Hadi hivi leo niko naye hapa mbele yako imepita miezi sita tangu tangu tumeonana au kuwasiliana. Huyu hapa leo, anahitaji nimsaidie.

Anahitaji msaada wa damu yangu, uhai wangu kumsaidia huyo mme wake. Ungekuwa wewe kaka ungemsaidia?